JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA


WAKALA YA SERIKALI MTANDAO

# eGA YAJA NA MFUMO WA KIELEKTRONI WA KUSIMAMIA UTENDAJI KAZI NA RASILIMALI ZA TAASISI KWENYE DIRISHA MOJA

Katika zama hizi za Habari, matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano hayaepukiki katika kuboresha utekelezaji wa shughuli za Serikali na hata katika sekta binafsi. Bila shaka TEHAMA imekuwa ni nyenzo muhimu na chachu ya kuongeza ufanisi katika ubunifu wa utoaji wa huduma kwa umma, kupata manufaa zaidi na kuwa sambamba na ulimwengu wa uchumi wa pamoja.

Kutokana na maendeleo ya Sayansi na Teknolojia, TEHAMA imekuwa nguzo muhimu zaidi katika kuboresha utendaji kazi wa taasisi mbalimbali zikiwemo za umma. Mkutano wa Dunia kuhusu Habari (World Summit of Information Society-WSIS)," uliofanyika mjini Geneva nchini Uswizi, mwezi Desemba mwaka 2003 na kuhudhuriwa na Wakuu wa Nchi na Serikali wa Afrika, umehimiza taasisi za umma kutumia TEHAMA ili kuchochea na kukuza maendeleo ya wananchi wao na taifa kwa ujumla na kuhakikisha jukumu la utoaji huduma kwa umma linafana.

"Tanzania mpya inakuja." Maneno haya machache na mazito ya Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, yaliyokuwa sehemu ya salamu zake za mwaka mpya, yalitoa changamoto kwa watanzania hasa watumishi wa umma kuwa wabunifu ili kuhakikisha maono yake yanatimia.




*Ukurasa wa mwanzo wa Mfumo Shirikishi wa Kusimamia Shughuli na Rasilimali za Taasisi (ERMS).*

Naye Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Dkt. Mary Mwanjelwa, katika ziara yake rasmi katika Ofisi za Wakala ya Serikali Mtandao Kanda ya Dar es Salaam, aliwataka watumishi wa umma kufanya kazi kwa bidii, uadilifu, uzalendo na uaminifu katika kubuni mifumo inayoboresha utendaji kazi Serikalini ili kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Mtendaji Mkuu wa Serikali Mtandao Dkt. Jabiri Bakari, anasema Wakala imekuwa mstari wa mbele katika kutumia TEHAMA katika shughuli zake za kila siku. Hii inaonekana katika jitihada za kubuni, kutengeneza na kutumia mifumo mbalimbali ya TEHAMA kitaasisi au kwa matumizi ya pamoja na taasisi za umma. Kwa kufanya hivyo, inatimiza Dira na Dhamira zake kwa kuratibu na kusimamia utekelezaji wa serikali mtandao na hivyo kutimiza ndoto ya Serikali ya Awamu ya Tano inayokusudia kuhakikisha kuwa utendaji kazi Serikalini na utoaji wa huduma kwa umma unaboreshwa.

"Ninatambua kuwa ni jukumu la Wakala kubuni mifumo mbalimbali ya TEHAMA ili kuiewezesha Serikali kutoa huduma za moja kwa moja kwa umma kwa haraka na kwa gharama nafuu" anasema Dkt. Bakari.



*Mtendaji Mkuu wa Wakala ya Serikali MtandaoDr. Jabiri Bakari akiongea na waandishi wa habari kuhusu Mfumo wa ERMS unavyofanya kazi, wakati wa mkutano na waandishi hao hivi karibuni jijini Dodoma*

Dkt. Bakari anaongeza kuwa moja kati ya mifumo muhimu iliyobuniwa, kusanifiwa na kutengenezwa na Wakala ni Mfumo Shirikishi wa Kusimamia Shughuli na Rasilimali za Taasisi (ERMS). Mfumo huu unatumika kusimamia shughuli za ndani za taasisi kwa kutumia moduli zinazowasiliana na kuunganisha shughuli za Idara na Vitengo. Aidha, mfumo huu umetengezwa mahususi kwa ajili ya matumizi ya Wakala pia unaweza kutumiwa na taasisi nyingine baada ya kuhuishwa kulingana na mahitaji ya taasisi husika.

"Lengo letu ni kuwa na dirisha moja ambalo linaunganisha mifumo mbalimbali ya kiutendaji ndani ya taasisi ili kuoengeza ufanisi, na wakati huo huo kupunguza gharama za uendeshaji na hivyo, kutoa huduma bora". Anasisitiza Dkt. Bakari.

Aidha, mfumo wa ERMS unasaidia kusimamia matumizi mazuri ya rasilimali na kuboresha utendaji kazi. Mfumo huu una moduli kumi na nane (18) zinazohusu shughuli mbalimbali za utendaji kazi katika taasisi ambazo zinawasiliana na kuweza kubadilishana taarifa miongoni mwa Idara/Vitengo. Moduli hizo ni:

Mipango, Bajeti, Uhasibu, Usimamizi wa Wateja, Usimamizi wa Huduma, Utoaji Ankara, Usimamizi wa Rasimaliwatu, Usimamizi wa Likizo, Usimamizi wa Miradi, Usimamizi wa Majukumu ya Watumishi, Usimamizi wa Ununuzi, Usimamizi wa Mali, Usimamizi wa Vitendeakazi, Usimamizi wa Vyombo vya Usafiri, Usimamizi wa watumiaji wa mfumo, Usimamizi wa Taasisi, Usimamizi wa Mfumo wenyewe, na Ripoti.

Dkt. Bakari anafafanua zaidi kuhusu moduli za mfumo wa ERMS akianzia na Moduli ya Mipango inayotumiwa kuwasilisha mpango kazi wa shughuli kwa ajili ya utekelezaji wa mwaka husika na ukamilishaji wa madhumuni na malengo ya kimkakati ya taasisi. Moduli hii inawezesha uwekaji wa vipaumbele vya malengo katika kipindi husika, pia hutumiwa na Wakuu wa Idara na Vitengo katika kutayarisha mpango kazi.

Akifafanua zaidi kuhusu moduli hizo, Dkt. Bakari anaelezea moduli ya Uhasibu kuwa ni moduli inayotunza kumbukumbu za fedha zilizopokewa na kutumika kwa mujibu wa matakwa ya sheria ya fedha za umma na miongozo ya uendeshaji taasisi. Anaongeza kuwa, moduli hii pia inawezesha utunzaji wa kumbukumbu mbalimbali za fedha kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vya utoaji wa taarifa za fedha katika sekta ya umma (International Public Sectors Accounting Standards (IPSAS). Zaidi ya hayo, moduli hii ina moduli ndogo sita (6) ambazo ni matumizi, memo ya kuweka na kutoa, mapato, karadha, usimamizi wa Taslimu, na marekebisho mengine.

Ameongeza kuwa moduli nyingine ni ile ya Usimamizi wa Likizo inayomuwezesha Afisa wa Rasilimaliwatu kushughulikia maombi ya likizo na ruhusa mbalimbali, na kufuatilia ruhusa zilizotolewa, zikiwemo likizo za mwaka, likizo ya ugonjwa, safari, pamoja na masuala binafsi, na kwa kutunza ratiba ya likizo.

Hali kadhalika kuna moduli ya Usimamizi wa Miradi, inayotumika kutunza kumbukumbu za miradi katika kipindi husika, ikionesha rasilimali zinazohitajika, hatua zilizofikiwa, na ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi hiyo. Pia, kuna moduli ya usimamizi wa majukumu ya watumishi ambayo ni mahususi katika kusimamia utekelezaji wa majukumu yao na kuwezesha ufuatiliaji wa utendaji wa kila mtumishi. Pia inawezesha upangaji wa majukumu na kutoa tathmini ya utendaji. Anaeleza Dkt. Bakari.

Moduli nyingine ni ile ya usimamizi wa ununuzi inayowezesha ufuatiliaji wa utekelezaji wa shughuli za ununuzi za taasisi kwa mujibu wa sheria ya ununuzi wa umma na kanuni zake. Moduli hii inawezesha utayarishaji wa mpango wa ununuzi wa mwaka, utunzaji wa taarifa za mali zilizonunuliwa, na usimamizi wa mikataba ya ununuzi. Moduli hii inaweza kuunganishwa na mfumo wa Taifa wa ununuzi (e-Procurement).

Zaidi ya haya, kuna moduli ya Usimamizi wa Mali inayosimamia mali za taasisi. Hali kadhalika, inafuatilia muda wa matumizi wa mali kwa kuzingatia hali, mahali ilipo, mtumiaji na kiwango cha uchakavu kwa kila mali. Moduli nyingine ni ya usimamizi wa Vitendea Kazi ambayo inawezesha kutunza kumbukumbu na ufuatiliaji vitendea kazi vya taasisi kwa kuzingatia hali, ratiba ya matengenezo na gharama. Moduli ya usimamizi wa Vyombo vya usafiri ni miongoni mwa moduli zilizopo katika mfumo huu ambayo inatunza kumbukumbu za magari na pikipiki ikihusisha gharama za matengenezo, ukarabati, jina la dereva na ofisa wa kila gari na pikipiki. Moduli hii pia inamuezesha mtumishi kuomba gari au pikipiki kwa kazi za ofisi. Anasema Dkt. Bakari.


Aidha, kuna Moduli ya Usimamizi wa Watumiaji wa mfumo, ambayo hutumika kwa ajili ya kutunza na kupanga majukumu na mipaka ya kila mtumiaji aliyeidhinishwa kutumia mfumo huo. Kwa upande mwingine kuna moduli ya kusimamia taasisi ambayo inatunza taarifa kuhusu taasisi ambazo ni wateja wa taasisi husika. Anafafanua Dkt. Bakari.

Aidha, anaeleza kuwa, mfumo huu unaruhusu kuongeza au kupunguza moduli kwenye mfumo mkuu bila kuathiri utendaji wa moduli nyingine. Moduli zote za mfumo huu huwa na muonekano wa aina moja na hivyo kuwa rafiki kwa watumiaji na hatimae hupunguza gharama za mafunzo.

Mfumo huu pia una moduli ya Bajeti inayowezesha kushughulikia matumizi ya fedha kwa mujibu wa shughuli zilizopangwa kwa mwaka husika. Moduli hii inawezesha kuonyesha gharama za shughuli na vifungu vya bajeti kwa watumiaji kwa ajili ya utekelezaji. Vilevile, inawezesha ugawaji wa fedha katika vifungu vya matumizi kwa mujibu wa kiasi cha fedha kilichopo. Sehemu hii ina moduli ndogo nne ambazo ni makisio ya mapato, bajeti ya Matumizi, Maombi ya Fedha, na Ugawaji na Usimamizi wa Fedha. Anaeleze Dkt. Bakari.

Pia, kuna moduli ya usimamizi wa Mteja inayotumika kutunza na kuweka kumbukumbu za mteja kwa kuongeza au kuhariri taarifa za mteja. Aidha, ipo Moduli ya kusimamia huduma zinazotolewa na taasisi kwa wateja wake inayoonesha orodha ya huduma mbalimbali zinazotolewa na taasisi. Moduli hii ina moduli ndogo nne ambazo ni: orodha ya huduma, bidhaa, maombi ya huduma, na malipo ya huduma. Ameongeza Dkt. Bakari.

Moduli nyingine ni ile ya utayarishaji Ankara. Anasema inatumiwa kuchanganua na kukokotoa gharama ya huduma zilizoombwa na wateja. Mbali na hiyo, pia kuna moduli ya usimamizi wa rasilimaliwatu kwa taasisi inayojumuisha utunzaji wa taarifa za utumishi za kila siku na kutoa ripoti mbalimbali.




*Dashibodi ya Mfumo Shirikishi wa Kusimamia Shughuli na Rasilimali za Taasisi (ERMS).*

"Tunaweza kusema kuwa mfumo wa ERMS, umetengenezwa hususani kwa matumizi ya taasisi ili kuongeza ubora wa huduma, kupunguza gharama za utendaji, kuwezesha matumizi bora ya rasilimali, kuwezesha utawala shirikishi na uwajibikaji". Anaeleza Dkt. Bakari

Naye Mkurugenzi wa Usimamizi wa Huduma za TEHAMA wa eGA, Injinia Benedict Ndomba anafafanua zaidi kuwa mfumo wa ERMS una dashibodi inayowawezesha Watendaji Wakuu na Watumiaji wengine wa mfumo huu kutayarisha na kutoa taarifa mbalimbali kulingana na mahitaji yao, kama vile taarifa za fedha, vifungu vya bajeti, bakaa ya fedha, hali ya matumizi ya rasilimali/fedha, tathmini za utendaji wa watumishi za kila siku ambazo huwawezesha kufanya uamuzi sahihi katika usimamizi na uendeshaji wa shughuli za taasisi.

Aidha, mfumo wa ERMS umebuniwa na kutengenezwa katika hali ambayo unaweza kuunganishwa na kubadilishana taarifa na mifumo mikuu ya Serikali kama vile mfumo Mkuu wa Fedha, Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Watumishi (HCMIS), Mfumo wa Malipo ya Serikali Kielektroni (GePG), Mfumo wa Baruapepe Serikalini (GMS) na Mfumo wa Ofisi Mtandao (GeOS). Pia ERMS inaweza kuunganishwa na kubadirishana taarifa na mifumo miingine yenye viwango vinavyokubalika kimataifa. Anaongeza Inj. Ndomba.

"Utengenezaji wa Mfumo wa ERMS unaonesha uzoefu wetu mkubwa wa utaalamu tulionao katika TEHAMA, ambao pia unaonesha mwanga wa matumaini na ustawi wa baadaye katika maendeleo ya utekelezaji wa serikali mtandao. Anasisitiza Dkt. Bakari.

Hivyo basi, anazitaka taasisi za umma ziendelee kutengeneza mifumo ya TEHAMA kwa kuzingatia viwango na miongozo ya Serikali Mtandao iliyopo na inayotolewa mara kwa mara ambayo hupatikana kwenye tovuti ya Wakala (www.ega.go.tz). Tunachohitaji ni stadi sahihi, kujiamini na kuzingatia matokeo bora. Wakala ya Serikali Mtandao itaendelea kutoa ushauri na msaada wa kiufundi kuhusu serikali mtandao kwa taasisi za umma.




*Mkurugenzi wa Usimamizi wa Huduma za TEHAMA wa Wakala ya Serikali Mtandao Injinia Benedict Ndomba akielezea jinsi matumizi ya TEHAMA yanavyoboresha utendaji kazi Serikalini wakati wa Kikao Kazi cha pili cha Serikali Mtandao kilichofanyika UDOM-CIVE tarehe 30 /01- 2 /02/ 2019*

Aidha, Dkt. Bakari anazihimiza taasisi za umma kutumia TEHAMA kwenye shughuli zao za kila siku kwa sababu ni kiungo kitakachoifikisha nchi yetu katika ngazi za juu za maendeleo ya viwanda yatakayo chochea maendeleo endelevu ya uchumi-jamii, kwa kuzingatia kuwa sekta zote za uchumi zinahitaji ubunifu katika TEHAMA.